# Shule za Msingi mkoani Dar es Salaam:

## Msongamano wa wanafunzi bila vitabu vya kiada vya kutosha

### Matokeo muhimu

- Msongamano wa wanafunzi madarasani ni mkubwa katika shule nyingi, kukiwa na wastani wa wanafunzi 81 katika darasa moja.
- Asilimia 45 ya shule zilizotafitiwa hazina madawati ya kutosha na wanafunzi wengi wanakaa sakafuni
- Upatikanaji wa vitabu vya kiada ni changamoto kubwa

*"Ingawa hivi karibuni Tanzania ilipewa tuzo na Umoja wa Mataifa kwa kuongeza uandikishwaji wa wanafunzi katika shule za msingi, ubora wa elimu inayotolewa ni wa kusikitisha"* [Tafsiri yetu] —The Citizen, 19 Oktoba 2010.

## Utangulizi

Tangu mwaka 2002, Serikali ya Tanzania imekuwa ikitekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) wenye madhumuni mawili makuu: kupanua zaidi upatikanaji wa elimu na kuinua viwango vya ubora wake. Wakati ambapo mafanikio makubwa yamepatikana katika kupanua upatikanaji wa elimu ya ngazi ya msingi, suala la kuinua viwango vya ubora bado linaendelea kuwa changamoto kubwa.

Dar es Salaam ni jiji kubwa kuliko miji yote nchini, na ni jiji lililo karibu zaidi na mahali sera zinapotungwa, hivyo mara nyingi inafikiriwa kuwa hali katika jiji hili ni bora zaidi kuliko mahali pengine. Hata hivyo, vyombo vya habari vimekuwa vikichapisha taarifa zinazotoa ushahidi unaoonesha kuwa shule za Dar es Salaam hazina vifaa vya kujifunzia na kufundishia na kwamba kuna haja kubwa ya kurekebisha hali hiyo. Kutokana na hali hii, Uwazi ilifanya utafiti kati ya mwezi Agosti na Desemba 2010 uliotathmini ubora wa huduma na vifaa/nyenzo katika sampuli ya shule za msingi 40 katika manispaa tatu za Dar es Salaam: Ilala, Kinondoni, na Temeke.

Taarifa zilizokusanywa katika utafiti huo zinaonesha kwamba, kinyume na dhana iliyoenea miongoni mwa watu, shule za Serikali jijini Dar es Salaam zinakabiliwa na changamoto kubwa katika upatikanaji wa vifaa vyenye ubora wa kufaa na vya kutosha kwa wanafunzi. Madarasa yaliyo duni na yasiyotosha, idadi ya madawati isiyokidhi mahitaji, na ukosefu wa vitabu vya kiada ni mambo ya kawaida katika shule za mkoa huu. Uwazi inaamini kwamba changamoto nyingi kati ya hizi zinaweza kutatuliwa, lakini kufanya hivyo kutahitaji kwanza wananchi wayaelewe matatizo haya, na wapate jukwaa au fursa itakayowawezesha kushiriki kikamilifu na kuchangia katika mijadala yenye lengo la kuinua viwango vya ubora katika shule.

Uwazi pata picha kamili

Muhtasari huu umeandaliwa chini ya uangalizi wa Rose Aiko wa Uwazi iliyopo Twaweza –Hivos Tanzania.


Uwazi, S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Baruapepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org
Umetolewa Mei, 2011.

Twaweza ni sisi

## Jambo la 1: Kuna msongamano mkubwa katika madarasa ambao husababisha mazingira duni kwa kujifunza

Wastani wa idadi ya wanafunzi kwa kila darasa katika shule zilizotafitiwa ni 81. Idadi hii ni kubwa mno kuliko kiwango cha kitaifa cha wanafunzi 40 kwa darasa kilichokusudiwa kufikiwa katika mwaka 2010. Hata hivyo, kuna tofauti katika uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa miongoni mwa shule (tazama Kielelezo cha 1). Katika shule za msingi za Buguruni Viziwi, Gerezani, Uhuru Wasichana, na Muhimbili, idadi ya wanafunzi kwa darasa iko kati ya wanafunzi 13 hadi 45, idadi inayofanya angalau kuwepo mawasiliano yenye ufanisi kati ya mwalimu na wanafunzi. Shule ya Buguruni Viziwi, ambayo ni maalumu kwa wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia, ndiyo iliyoshinda shule nyingine kwa mujibu wa kuwa na idadi ndogo ya wanafunzi katika darasa, ikiwa na uwiano wa wanafunzi kumi kwa mwalimu mmoja (10:1).  Pamoja na udogo wa idadi ya wanafunzi kwa darasa, ambao ndiyo unaofaa ili kutimiza mahitaji maalumu ya wanafunzi, vilevile shule ina vifaa vyenye ubora mzuri ikilinganishwa na shule nyingi nyingine, shukrani nyingi kwa msaada wa kifedha kutoka kwa wahisani mbalimbali wanaothamini elimu ya watoto hawa. Hata hivyo shule nyingine kama vile Mbagala, Vijibweni, na Tandika (katika wilaya ya Temeke) na Bunju A na Kunduchi (katika wilaya ya Kinondoni) ziko katika upande mwingine wa mizani zikiwa na zaidi ya wanafunzi 130 kwa darasa. Shule za Vijibweni, Tandika na Bunju A zinajaribu kushughulikia tatizo hili kwa kufundisha Darasa la 1 na 2 kwa zamu au kupokezana nafasi.

**Kielelezo cha 1: Uwiano wa wanafunzi kwa darasa katika shule zilizotafitiwa**




**Chanzo cha Takwimu:** Uwazi, 2010.


Si madarasa yote katika shule zenye uwiano mzuri wa wanafunzi kwa mwalimu yako katika hali nzuri na inayofaa kwa kujifunzia. Kwa mfano, licha ya kuwa na wastani wa wanafunzi 41 kwa darasa, kiwango ambacho ni karibu ya kile kilichopendekezwa na Serikali, Shule ya Msingi Amana katika wilaya ya Ilala ni 'shule inayokufa'. Ikiwa imeanzishwa mwaka 1947, shule inaonekana kama kwamba haijafanyiwa matengenezo yoyote tangu ilipojengwa: kuta zake zimeota kuvu, zikiwa na rangi iliyochoka, na madirisha yake na dari vikiwa katika hali mbaya sana. Shule imebanwa katikati ya eneo la Ilala, kiasi kwamba ni vigumu kwa mgeni kutambua kuwa kuna shule mahali hapo. Idadi ndogo ya wanafunzi (wanafunzi 288) katika shule inaakisi jinsi wakazi wa eneo hili wasivyovutiwa na shule hii. Wazazi wengi wanachagua kuwapeleka watoto wao mahali pengine kwa kuwa mazingira katika shule ya Amana hayaonekani kuwa mazuri kwa watoto wao kujifunza.

> "Wakati mwingine kunakuwa na sauti kubwa ya muziki kutoka kwenye biashara zilizo maeneo ya jirani na pia makazi ya watu ambazo huwasumbua wanafunzi katika kujifunza," anasema mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi ya Amana. "Iwapo serikali inataka mahali hapa kuendelea kuwa shule, basi matengenezo makubwa yanahitajika au (hata) kujenga maghorofa mapya baada ya kuvunja haya yaliyopo".

## Jambo la 2: Katika nusu ya shule zilizotafitiwa, wanafunzi wanalazimika kukaa sakafuni

Kwa wastani, katika shule zilizotafitiwa, wanafunzi watano wanakaa katika dawati moja (lenye uwezo wa kukaliwa na wanafunzi watatu), huku kukiwa na tofauti kubwa kutoka shule moja hadi nyingine. Katika takribani nusu ya shule (18 kati ya 40) hapakuwa na madawati ya kutosha kwa wanafunzi wote na wanafunzi wengi wanalazimika kukaa chini (tazama Kielelezo cha 2). Kwa ujumla, shule zenye uwiano mkubwa wa wanafunzi kwa mwalimu mmoja ndizo pia zisizokuwa na madawati ya kutosha.

**Kielelezo cha 2: Je, wanafunzi wanakaa sakafuni?**





**Chanzo cha takwimu:** Uwazi, 2010.

Ukosefu wa madawati ni tatizo kubwa zaidi katika Shule ya Msingi Kunduchi. Kiasi cha robo tatu ya wanafunzi 1,931 katika shule hii hawana madawati, hali inayoonesha wazi kudhoofisha ubora wa elimu inayotolewa shuleni hapo. Bila kupata rasilimali kutoka Serikalini ili kusaidia shule kama hii, tegemeo pekee ni kwamba wadau wengine watabaini hali ilivyo na kuchangia kwa njia mbalimbali.

## Jambo la 3: Upatikanaji wa vitabu vya kiada ni changamoto kubwa

Upatikanaji wa vitabu vya kiada ni suala muhimu katika kujifunza. Hata hivyo, utafiti unaonesha katika shule nyingi hakuna vitabu vya kiada vya kutosha. Wastani wa uwiano ni wanafunzi 5 kwa kitabu kimoja katika madarasa ya chini ya shule za msingi na wanafunzi 6 kwa kitabu kimoja katika madarasa ya juu ya shule za msingi (tazama Kielelezo cha 3).

**Kielelezo cha 3: Uwiano wa wanafunzi kwa kitabu cha kiada katika shule za Dar es Salaam zilizotafitiwa**




**Chanzo cha data:** Uwazi, 2010.

Katika shule zilizotafitiwa, kuna tofauti kubwa kuhusu upatikanaji wa vitabu. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa Shule ya Msingi Mlimani yenye uwiano wa wanafunzi wawili kwa kitabu kimoja, ni moja kati ya shule zenye fursa nzuri zaidi ya kujifunza miongoni mwa shule zilizotafitiwa. Hali hii bora inatokana na wanafunzi wengi kuleta shuleni vitabu walivyonunuliwa na wazazi wao na haitokani na kwamba shule inagharimiwa vizuri zaidi na Serikali. Katika Shule ya Msingi Kunduchi, uwiano wa

mwanafunzi kwa kitabu kwa shule yote na katika masomo yote ni wanafunzi 10 kwa kitabu kimoja (10:1); na katika Shule ya Msingi Tandika, uwiano katika madarasa ya juu ni wanafunzi 15 kwa kitabu kimoja (15:1). Shuleni Bunju A, kwa baadhi ya masomo uwiano uko juu sana kufikia 45:1. Akionesha hali mbaya zaidi, mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi Mbagala aliripoti kuwa katika madarasa yake ya juu, ni walimu tu ndiyo walio na vitabu. Kama ilivyo katika Shule ya Msingi Mlimani, baadhi ya shule sasa zimeanza kushughulikia suala la vitabu miongoni mwao. Kwa mfano, kwa maelezo ya mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi Kunduchi, shule imewaomba wazazi wa wanafunzi walio katika madarasa ya 4 hadi 7 kuwanunulia watoto wao vitabu.

## Hitimisho

Ikiwa ni karibu muongo mmoja sasa tangu kuanzishwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), utoaji wa huduma na vifaa vya kutosha mashuleni kama vile vyumba vya madarasa, madawati, na vitabu vya kiada umebaki kuwa changamoto, hata katika jiji la Dar es Salaam. Kwa mujibu wa Takwimu za Msingi za Elimu (*Basic Education Statistics*) zinazoshapishwa na Wizara ya Elimu, inaonekana shule za msingi katika mkoa wa Dar es Salaam zinahudumiwa vizuri zaidi kuliko shule nyingi katika mikoa mingine nchini. Mathalani, katika wilaya ya Temeke, katika mwaka 2009, uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu uliripotiwa kuwa wanafunzi 46 kwa mwalimu mmoja (46: 1), ambapo wastani wa taifa ulikuwa wanafunzi 55 kwa mwalimu mmoja (55:1). Kinyume chake, wastani wa uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu katika wilaya ya Geita mkoani Mwanza, wilaya iliyo mbali sana na Dar es Salaam, ulikuwa wanafunzi 78 kwa mwalimu mmoja (78:1). Iwapo vifaa na huduma katika wilaya zenye rasilimali zaidi si za kuridhisha, kama inavyooneshwa katika muhtasari huu, basi kuna wasiwasi mkubwa kuhusu elimu ya wanafunzi walioko katika wilaya zinazopata rasilimali kidogo zaidi.

**Kiambatisho: Shule za msingi za Serikali zilizotembelewa katika utafiti**

| Wilaya ya Temeke (16) | Wilaya ya Ilala (13) | Wilaya ya Kinondoni (11) |
|---|---|---|
| Vijibweni | Buguruni Moto Mpya | Kawe A |
| Mji Mwema | Boma | Kumbukumbu |
| Mivinjeni | Amana | Mapambano |
| Tua Ngoma | Buguruni Viziwi | Mbuyuni |
| Kibada | Msimbazi Mseto | Oysterbay |
| Chang'ombe | Gerezani | Kinondoni |
| Geza Ulole | Muhimbili | Msisiri |
| Mtoni Kijichi | Ukonga | Mlimani |
| Kimbiji | Buguruni Moto | Bunju A |
| Kurasini | Buguruni | Mtongani |
| Kibugumo | Mnazi Mmoja | Kunduchi |
| Tandika | Uhuru Wasichana | |
| Mgulani | Bunge | |
| Mikwambe | | |
| Kigamboni | | |
| Mbagala | | |

**Chanzo cha takwimu**

Muhtasari huu ni sehemu ya ufuatiliaji wa wananchi unaofanywa katika Uwazi, www.uwazi.org. Takwimu zimekusanywa kupitia utafiti wa ufuatiliaji ulioendeshwa kati ya Agosti na Desemba 2010. Takwimu zote zinaweza kupatikana kutoka Uwazi.